BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA NANE

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 22 Septemba, 2022.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2021/2022.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Ripoti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

67. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ:

    Naipongeza Serikali yetu kwa kuamua kwamba vijana wetu wanaomaliza masomo yao wapitie kwenye kambi za Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kwa lengo la kujitolea kabla ya kupatiwa ajira rasmi. Hata hivyo, matayarisho ya vijana hao wakiwa

makambini hayaoneshi kukidhi haja ya maamuzi husika ya Serikali ya kuwepo kwao katika kambi hizo.

(a) Je, katika kujitolea kwao vijana hawa hasa hupangiwa kufanya shughuli gani.

(b) Je, ni kwa nini Serikali isiwaandalie mazingira ya kuwapatia mafunzo ya amali kwa kiasi kikubwa makambini humo ili wakitoka wawe na uwezo wa kujiajiri wenyewe na kuajiri wengine.

<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>

131. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni moja wapo kati ya wamiliki wa iliyokuwa Benki ya Posta ambayo kwa sasa inajulikana kwa jina la Benki ya Biashara ya Tanzania “Tanzania Commercial Bank”.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimewekezwa katika Benki hiyo.

(b) Je, ni kiasi gani cha faida ambacho kimepata au inapata Zanzibar katika uwekezaji huo.

<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>

16. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kuna tatizo kubwa linaloendelea kujitokeza siku hadi siku katika maeneo mengi ya kupokelea wageni kama vile viwanja vya ndege vya Zanzibar. Wageni wanapokuja kuchukuliwa na wenyeji wao hulazimika kusubiria dereva aende dirishani kupeleka kadi kwa lengo la kufanya malipo ili apewe kadi ya kutolea gari

(a) Je, Wizara yako haioni kuwa utaratibu uliopo hivi sasa unaleta kero kwa abiria na hata kwa wenyeji ambao wamefika kuwafuata wageni wao.

(b) Kwa nini Wizara isiweke utaratibu maalumu wa malipo kwa madereva wakati wakifika uwanjani kusubiria wageni wao.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

120. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa tunavishuhudia viwanja vingi vya mpira nje ya nchi yetu vikiwa na huduma mbali mbali za biashara kwa kujengwa maduka pembezoni na kusaidia upatikanaji wa mapato ya ziada. Na kwa kuwa viwanja vyetu vya mpira Amani na Gombani vinayo maeneo ya kutosha pembezoni kufanya shughuli hiyo.

Je, kwa nini Serekali haibuni uwekaji wa maduka makubwa ya biashara na huduma pembezoni mwa viwanja hivyo, ili kuviongezea thamani ya mapato kibiashara.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

8. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAKA KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Maeneo mengi yaliyochimbwa mchanga na kifusi yamebaki kuwa ni mashimo ya muda mrefu na kupelekea haiba ya asili ya maeneo hayo kupotea.

Je, Serikali imejipanga vipi kurejesha haiba ya maeneo hayo.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

112. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kumekuwa na ongezeko la idadi ya watoto wanaopotea wenyewe au kuibiwa ndani ya visiwa vya Unguja na Pemba.

(a) Je, ni idadi gani ya watoto waliopotea wenyewe au walioibiwa na kushindwa kupatikana kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita.

(b) Je, ni zipi juhudi za Serikali katika kuliondoa janga hilo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

54. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wizara yako kwa kipindi kirefu imekuwa na utaratibu wa kuzalisha mimea chotara (Hybrid plants) kama vile miembe, minazi na mihogo. Hata hivyo, baada ya kufanya utafiti wa kina, imegundulika kuwa zao kubwa la biashara kwa maana ya mkarafuu hadi leo hii bado halijawa na mmea wake chotara kama ilivyo kwa mimea mengine.

Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea kukosekana kwa mimea chotara ya mikarafuu jambo linalopelekea kuendelea kutumia mikarafuu asilia hadi leo hii.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

109. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Wananchi wengi walisikitika pale walipowaona wanafunzi wa skuli ya Tumekuja wakihama skulini hapo mnamo mwezi wa Julai 2022, wakiwemo wale ambao wanakabiliwa na mitihani ya taifa, mwezi Oktoba mwaka 2022 bila ya matayarisho yanayoridhisha katika skuli walizohamia.

(a) Je, wanafunzi hao wako katika mazingira gani hivi sasa katika skuli walizohamia.

(b) Je, Serikali inachukua juhudi gani kuhakikisha kwamba watafanya mitihani yao ya taifa katika mazingira sawa na wenzao bila ya kuathiri ufanisi wao.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

Ripoti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa mwaka 2021/2022.

Zanzibar,
22 Septemba, 2022.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.